
# UTOWAJI MIMBA KWA KUTUMIA VIDONGE VYA

## MIFEPRISTONE NA MISOPROSTOL (MUCHANGANYIKO)



## NGUVU YA DAWA

Muchanganiko wa MISO na MIFE ni salama na kamilifu kwa kiwango makumi kenda na tano hadi makumi kenda na munane za kesi kwa miya (95-98%) muma inga kumi na mbili (12) za mwanzo wa mimba.

## NINI IFANYIKE IKIWA MIMBA AIKUTOKA?

Mwanamuke anaweza kurudiliya kutumiya dawa MIFE – MISO ao kutumiya mutindo wa kununusa mimba (aspiration). Kuna hatari ndogo sana ya ulemavu wa fetasi (fœtus) ikiwa mimba inaendeleya kisha kutumiya dawa.

## JE, MIMBA YANGU IMEFANYIKIWA KUTOKA ?

**Hata ikiwa mwanamke anajisikia kwamba hana tena mimba, ni muhimu kuhakikisha kama kweli mimba ilitoka. Inabidi kufanya kipimo cha echographia, baada ya kutowa mimba kwa njia ya vidonge, au kipimo cha mimba baada ya inga 3 au 4 kwa kuhakikisha kama ilitoka kweli-kweli.**

Ikiwa mwanamuke hatoki damu, anatoka damu kidogo (kuliko munzunguuko wa hedhi na hana mabonge ya mimba) na / ao dalili za mimba zaendeleya baada ya kukunywa dawa, ya wezekana mimba yaendeleya. Ni vema afanye ultrasound échographie) haraka iwezekanavyo kwa kuhakikisha kama mimba yaendelleya ao apana, ikiwa mimba yaendeleya anaweza tena kukunywa dawa kwa mara ingine.

## BAADA YA MIMBA KUTOKA

Baada ya mimba kutoka, mwanamke anaweza kuendelea kutoka damu kidogo kidogo kwa mda wa juma 1 au 3, lakini inafuatana na hali ya mwanamke. Ya maana ni kuhakikisha kama mimba inatoka bila tatizo.

Aupashwi kuingiza kitu chochote kile ndani ya uchi ya mwanamke wako ( mfano pamba) au kufanya ile bain ya zaidi, au kufanya tendo la ndoa na mwanamme, mpaka ile damu iwe yenye kupunguka karibuni siku mbili (2) hivi kisha mimba kutoka kupitiya vidonge.

**Mwanamke anaweza pata ingine mimba palepale baada mimba kutoka!** Kwa kuepuka kubeba mimba ya haraka baada ya mimba kutoka, nilazima kutafufa mpango wa uzazi uliyo bora.

## CONTACTS

Women HelpWomen
WEB: HTTPS://WOMENHELP.ORG/
EMAIL: INFO@WOMENHELP.ORG
TWITTER: @WOMENHELPORG
FACEBOOK: WOMENHELPWOMENINTERNATIONAL

MAMA Network: Mobilizing Activists around Medical Abortion (MAMA).
WEB: WWW.MAMANETWORK.ORG

## INAFANYA JE (INATEMBEA JE) ?

Matumizi ya misoprostol inafanana moja kwa moja na ile ya mimba kuharibika.

MIFEPRISTONE MISOPROSTOL

Mifepristone uzuiya progestérone, mboleo ambayo usaidia mimba kuendelea na kusaidia kizazi kujitayarisha kupokea Misoprostol.

Vidonge vya Misoprostol vinaleta maumivu kidogo kidogo ndani ya kiungo cha uzazi ambao husababisha kupasuka kwa colle, kufunguka na kuanza kutoka damu.

## KWA WAKATI GANI HIYI (MISO ET MIFE) YAWEZA KUTUMIKISHWA KWA UTOWAJI MIMBA KAMILIFU ?

0 ≫12 wiki

Munamo inga kumi na mbili (12) ya mimba, tangiya siku ya kwanza ya muzunguuko wa hedhi wa mwisho.

## JINSI GANI UTUMIKISHE DAWA KWA KUTOA MIMBA KAMILI ?

MIFEPRISTONE 200 mg — MISOPROSTOL 200mg kila kimoja

Mwanamke atakuwa na lazima ya kidonge kimoja (1) cha Mifepristone ya 200 mcg na ingine ine (4) ya Misoprostol ya 200 mcg kila kimoja.

MIFEPRISTONE 200 mg +

**Mifepristone** inapashwa kumezwa na kopo moja ya maji (verre moja).

Kisha saa 24, weka/tia **vidonge 4 vya misoprostol** ndani ya kinywa.

24 saa

Tiya vidonge mbili kwenye pembe ya meno na machafu yani mbili kushoto na mbili kuume

**Vidonge 4 vitabaki ndani ya kinywa mda wa dakika 30** ukimeza mate tu hadi vimalizike, baada ya dakika hizo, mwanamke anaweza kunywa maji akimeza yale mabaki. Baada ya hapo mwanamuke anaweza meza masaliyo (ao mabaki).

30 dakika

## UWEZEKANO WA MATOKEO/VINYUME VINGINE



24h

Baada ya masaa 24 kisha kutumia dawa (vidonge), hali kama hizi zinaweza zikafike : kichefuchefu, kutapika, kuharisha, homa ya 38°, kichwa kuuma na mchoko, dalili hizo siyo za kusumbua sana na zinaisha kwa masaa kidogo tu.



## NINI INAWEZA TOKEA BAADA YA KUTUMIA MISOPROSTOL?

Maumivu mengi na kuvuja damu nyingi kupita damu ya kawaida.

24 saa

Munamo makumi kenda ya kesi kwa miya (90 %) mimba ya rushwa ndani ya ma saa sita za mwanzo.

Jinsi mimba inakomaa zaidi (kukuwa), ndivyo hivyo mwanamke atavuja damu.

Dawa zakutuliza maumivu zaweza kukamatiwa kwa kiwango cha mwazo pamoja na Misoprostol. **Ibuprofen** ya saidiya zaidi piya, **paracetamol** ya wezwa kuhongezwa.

## ALAMA GANI ZA KUTATANISHA ?

- utoka damu kupita kiasi (hadi unajaza cotexte 2 au 3 kwa saa moja zaidi ya saa 2 au 3 kufwatana)2h +
- 39° Homa kali (zaidi ya 39°) au 38° kwa mda wa zaidi ya ma saa 24 (24h +)
- Maumivu makali isiyomalizika ijapokuwa unakunywa dawa za kupunguza maumivu siku za kufuatana baada ya kukamata dawa
- Kutokwa na vitu vibaya ndani ya uchi na vyenye harufu mbaya.

## IFANYIKE NINI IKIWA KUNA MATATIZO

**Wende mara moja kwenye kituo cha afya kilicho karibu**

Ikiwa mwanamke ana lazima ya matunzo, mganga anapashwa kumtunza. Matunzo ya utoaji mimba kwa njia ya vidonge iliyosababisha matatizo inalingana sawasawa na yale ya mimba kuaribika. Ni vigumu kutofautisha mimba ambayo imearibika na ambayo ilitoka kupitia vidonge vya Mifepristone na Misoprostol. Inamaana kwamba mwanamke anapokuwa na lazima ya matunzo anawezasema kama mimba iliaribika.